

Ni asubuhi yenye kupendeza jua likiwa limechomoza kuashiria siku nyingine imewadia.Noel alikuwa amebeba begi lake mgongoni akielekea shuleni lakini alionekana kuwa ni mtu mwenye mawazo mengi sana, nyuma yake Mzee mmoja alikuwa anakuja akiendesha baiskeli akiwa anapiga mluzi.

Kwa bahati mbaya alikuwa anapita karibu zaidi na upande aliokuwepo Noel, akamkwaruza na baiskeri yake sehemu ya mguuni.Noel hakuongea chochote, alikaa kimya ‘kijana samahani’ alisema yule Mzee huku akishuka taratibu kutoka kwenye baiskeli yake, ‘bila samahani Mzee wangu’ alisema Noel, akiendelea kutembea lakini anachechemea kidogo kwa kuwa alipata maumivu ya wastani.

Yule mzee alipo mwangalia usoni, aligundua kuwa ni mtu mwenye msongo wa mawazo. ‘Lakini mbona una mawazo sana kijana wangu?’, aliuliza yule Mzee lakini Noel akawa mzito kidogo kuongea.

‘Hamna Mzee’ aliongea akionyesha uso wa tabasamu kijana Noel ‘punguza mawazo, mawazo ya nini wewe ungali kijana mdogo!’ alisema yule Mzee mwenye baiskeli kisha aliondoka na kumuacha Noel akiwa amesimama njiani.

Noel alikuwa mwanafunzi wa kidato cha sita katika shule ya sekondari ya Mwanza, alitokea katika familia ya watu wa maisha ya chini.

Mama yake alikuwa anauza pombe za kienyeji na Baba yake alikuwa amewatelekeza tangu walipokuwa waangali watoto wadogo, ‘maisha haya najua ipo siku nitaondokana nayo’ aliwaza akilini mwake kisha akaondoka na kuelekea darasani. Noel alikuwa na ndoto kubwa katika mpangilio wa maisha yake, mara nyingi aliwaza ipo siku moja atakuja kuwa mwandishi mzuri wa vitabu.

Lakini pia alipenda kutoka katika maisha ya umasikini.‘Noeli?’ alimuita msichana mmoja aliyekuwa anasoma nae, aligeuka na kuitikia kwa upole ‘naam’ huku akiwa bado angali amegeuza shingo yake kumtazama yule msichana.

Yule binti nae alikuwa amevaa sare nzuri za shule, daftari zake zilikuwa nadhifu alikuwa ameziweka katika mafaili aliyokuwa ameyashika mkononi, ‘duuuuh!Leo tumechelewa’ alisema yule binti.

‘Siku huwa hazilingani’ alisema Noel kwa utaratibu huku wakitembea mwendo sanjari na yule binti,‘kazi ya mwalimu ulifanya?’ aliuliza yule binti, ‘Mimi natamani tu kumaliza shule’ alisema Noel akiwa amekata tamaa na maisha ya nyumbani kwao ya kuuza pombe ya kienyeji.

Yumbani kwao hali ya biashara hiyo ilikuwa mbaya sana kutokana na polisi kumsumbua Mama yake kila siku, polisi walikuwa hawaishi kufika nyumbani kwao.

“Sijaifanya kazi yake” alisema Noel, “Mwalimu atakufukuza kwenye kipindi chake ”, aliongea yule Binti akimsikitia Noel.

“Baadae nitaifanya” alisema Noel, uwezo wa masomo ya darasani alikuwa nao mkubwa lakini tatizo ni umasikini uliokuwa umekithiri alimuathiri saikolojia yake. Noel kila siku jua linapozama na kuchomoza alikuwa akiwaza atafanya nini ili aweze kulipa deni alilokuwa anadaiwa shuleni.

”Dah! Maisha magumu”, aliongea huku anashusha pumzi yake kwa nguvu. Kila ngazi ya elimu aliyokuwa akipitia alikutana changamoto nyingi sana.

Walianza kuingia katika eneo la shule, kwa mbali walianza kuona walimu wakiwa wamesimama na mhasibu wa shule. Pamoja na kuwa mbali lakini walimu walikuwa wameshamuona Noel “hivi huyu kijana amegoma kutoa pesa?” aliuliza Mwalimu mmoja. “Sijui naona yuko kimya”, waliendelea kumjadili Noel.

Kila siku Noel alikuwa anaitwa ofisini kwa Mhasibu, kusoma kwake kulikuwa kwa mashaka hakuwa na furaha hata kidogo. Aliishi kwa wasiwasi muda wote alipokuwa shuleni. ”Nitaifanyeje, nitaifanyeje?”, ndio lilikuwa swali lake kila mara kijana Noel. Alipokuwa akitembea kuelekea shuleni alifika sehemu yenye uwazi ambapo walionekana, Walimu wake wakamuita kwa sauti “Noeli?”

“Nammm Mwalimu?”, aliitikia kwa upole akiwa anageuza shingo yake, alikuta ni wale walimu wake ambao kila siku walikuwa wanamsumbua shuleni kutokana na madeni aliyokuwa nayo. ”Aiseee narudi nyumbani” ndilo wazo aliloliwaza kwa haraka wakati huo Noel.

Licha ya kupitia mambo yote hayo, lakini bado Noel aliamini kuwa ipo siku matatizo yataenda kuisha, ”Wewe fedha tunayokudai umelipa?” aliulizwa na Mhasibu wa shule.

“Hapana”, alijibu kijana Noel, Mwalimu Mkuu aliamua kutoa agizo kuwa Noel afukuzwe shule. “Mwalimu huyu aende nyumbani tu” aliongea akiwa amelishikilia begi la Noel.

Noel anafukuzwa kurudi tena nyumbani kwao, kufukuzwa kwa Noel ilikuwa imesha kuwa kawaida. Wanafunzi wenzake ilifikia hatua waliona ni jambo la kawaida kwa Noel kurudishwa nyumbani kutokana na madeni aliyokuwa anadaiwa.

Noel akiwa njiani aliawaza “nirudi tena nyumbani?”, alijiuliza swali hilo kichwani mwake kwa dakika kadhaa, mara anapata ufahamu wa haraka “ ngoja niende mtaani” aliwaza hivyo hatimaye aliamua kwenda mjini.

Rafiki yake alikuwa darasani akimsubiri, ”leo Noeli yuko wapi?” alijiuliza wenyewe tu akilini huku akiwa anajinyoosha. Rafiki yake Noel alionekana kutokufurahia somo la Mwalimu aliyekuwepo darasani wakati huo kwa maana mawazo yake yaikuwa juu ya rafiki yake.